# Usawiri wa Upembezaji wa Mwanamke katika Bunilizi za Clara Momanyi

*Kawira Kamwara*
*Chuo Kikuu cha Nairobi*

**Ikisiri**

**Makala haya yanahusu usawiri wa upembezaji wa mwanamke katika bunilizi za Clara Momanyi. Upembezwaji wa mwanamke ni suala ambalo limekithiri katika jamii nyingi za Kiafrika. Utamaduni hasi na ubabedume ni mambo ambayo yamechangia pakubwa upembezwaji huu. Hata hivyo, kwa kiwango fulani mwanamke mwenyewe amechangia hali hii kwa kujidunisha mwenyewe au kwa kukosa sauti na ujasiri wa kusimama kidete na kujiamulia mustakabali wake. Suala hili limejitokeza katika bunilizi za Clara Momanyi. Katika makala haya, nilihakiki hadithi fupi zifuatazo: '*Ngome ya Nafsi*' kwenye diwani ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (2004) na riwaya ya *Tumaini* (2006).**

**Istilahi Muhimu**: upembezwaji, Ufeministi wa Kiafrika, ubabedume, utamaduni na bunilizi

## Utangulizi

Dhana ya upembezwaji wa mwanamke ni hali ya kuwekwa pembeni na kutengwa. Pia, ni hali ya kutomhusisha mwanamke katika masuala yanayomhusu. Isitoshe, mwanamke anatengwa katika masuala ya kijamii na kukosa kupewa nafasi na majukumu. Hali ya upembezwaji wa mwanamke ni suala linalojitokeza kwa njia nyingi mbadala katika tafiti. Kwa mfano, Lugano (1989) anahoji kwamba, mwanamke amesawiriwa kuwa kiumbe duni chini ya utawala na uelekezi wa mwanamume. Hivyo, mwanamke anachorwa kama kiumbe anayemtegemea mwanamume. Usawiri huo unatuelekeza kwenye kauli kwamba Kezilahahi amesaidia kujenga ujitambuzinafsia wa kijinsia uliokitwa katika misingi ya uzalishaji, umiliki mali na utegemezi, japo athari hasi za utegemezi huo hazijabainishwa.

Muindi (1990) naye anadai kwamba ubaguzi wa kijinsia unaibua hali ya mwanamke kupembezwa kwa kutazamwa kama kiumbe duni katika jamii. Akimwangalia mwanamke katika miktadha ya ukahaba, Muindi anahoji kuwa umaskini unamsukuma mwanamke hadi kwenye ukahaba kwa sababu nyenzo za uzalishaji mali zinadhibitiwa na jinsia ya kiume. Katika hali hizi, kunajitokeza upembezwaji wa jinsia katika misingi ya kiuchumi. Kwa hivyo, panaibuka upembezwaji wa mwanamke wa kiuchumi kwamba, anaondolewa katika nyenzo

zilizo na tija na kusukumwa hadi miktadha ya kuchumia kijungu. Mwanamume anatwikwa majukumu na utamaduni; ya kufanya maamuzi kuhusu familia yake huku mwanamke akiachiwa uzazi na malezi. Ingawa mwanamke anajitahidi kushiriki katika maendeleo ya jamii, hunyimwa nafasi hiyo na kukumbushwa kuwa ni makosa kufanya kinyume na anavyotarajiwa. Ingawa jamii inampembeza mwanamke, mwanamke amefikia hali na hatua ya kutambua na kupigania haki yake katika jamii. Anakataa kufungwa kwa pingu za utamaduni na ubabedume. Mbali na hayo, Musyoka (2011) anatathmini mabadiliko katika jamii kuhusu ujenzi wa utambulisho wa jinsia kwa kuzingatia nadharia ya Ufeministi. Musyoka anahoji kwamba, ujenzi wa ujitambuzinafsia wa jinsia katika vipindi tofauti kihistoria unampembeza mwanamke kwa mujibu wa mazingira ya watunzi. Ingawa mazingira yanamwathiri mwanamke na kutazamwa kama kiumbe duni, mwanamke anasawiriwa kama kiumbe jasiri anayepinga upembezwaji na kutetea nafasi yake kama kiumbe stahiki katika jamii. Anatumia silaha ya akili aliyopewa na Mungu kujikomboa na kuonyesha kuwa, mwanamke hayuko tayari kuzidi kukandamizwa na kutumiwa vibaya.

Swaleh (2011) anaangazia mchakato wa ujenzi wa ujitambuzinafsia wa jinsia na upembezwaji wa mwanamke, Swaleh anahoji kuwa, mtunzi wa kazi ya sanaa anaongozwa na ada na tamaduni za jamii husika katika kubainisha mitazamo anayochukua mwanamke ambayo inamtambulisha katika jamii. Anabaini kuwa mwanamke anapigania nafasi yake kwa kupinga utamaduni kandamizi na desturi kama vile za tohara, ndoa za mapema na ubaguzi wa kijinsia. Uhakiki wa Swaleh kwa jumla unaonyesha kuwa upembezwaji wa mwanamke umeathiriwa pakubwa na tamaduni pamoja na mazingira anamokulia mwanajamii.Vigezo vya utamaduni na mazingira vimekuwa vimetumika katika ujenzi wa ujitambuzinafsia hasi kwa jinsia ya kike kwa mujibu wa jamii za watunzi wa bunilizi teule alizochanganua.Suala hili limesawiriwa na Momanyi katika bunilizi zake.

**Mtazamo wa Kinadharia**

Uhakiki huu umeongozwa na nadharia ya Ufeministi. Nadharia hii hulenga kuangazia masuala ya kijinsia katika jamii hasa kwa kujikita katika hali ya kumkomboa mwanamke dhidi ya unyanyasaji. Ni dhana inayopinga mielekeo ya mfumo wa ubabedume. Ni nadharia iliyoasisiwa na Wollstonecraft (1792) katika makala yake yaliyotetea ujenzi wa utambuzi wa jamii usiobagua wanajamii kwa misingi ya jinsia. Nadharia ya Ufeministi inaungwa mkono na Beauvoir (1949), anaposhambulia jamii kwa jinsi inavyojenga ujitambuzi hasi wa jinsia kwa kumpembeza mwanamke kupitia misingi ya asasi kama ndoa na utamaduni. Kwa kupitia mtazamo wa Beauvoir, utamaduni unaozingatiwa na jamii una nguvu ya aina fulani inayotumiwa kama kigezo cha kuiongoza.

Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (1999), nadharia hii huwa na matapo manne, mojawapo likiwa ni tapo la Ufeministi wa Kiafrika. Tapo hili huonyesha nia na malengo kuhusu hali halisi katika jamii za Kiafrika. Kulingana na hoja hii,

nadharia hii itatuongaza kuchunguza masuala ya kijinsia katika kazi teule ili kuafiki mielekeo ya kijamii kuhusu ujenzi wa ujitambuzi nafsia wa jinsia. Uhalisia wa maisha ya jamii ya watunzi utaweza kubainika kupitia kwa usawiri wa wahusika pamoja na mjukumu yoa. Vilevile, tutachunguza masuala ya kijinsia katika kubainisha hatua za ujenzi wa jamii mpya ambayo wanajamii wathaminiwa bila ubaguzi. Kauli hii itatusaidia kubaini ni kwa jinsi gani Momanyi anaangazia suala la upembezwaji wa mwanamke katika jamii. Hivyo, nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ndiyo imetumika katika kuhakiki suala hili.

### Tapo la Ufeministi wa Kiafrika

Tapo la Ufeministi wa Kiafrika lilizuliwa na Steady kwa mtazamo wa mwanamke wa Kiafrika mnamo 1981 ili kuangazia masuala ya kijinsia barani Afrika. Katika kitabu chake, anasema kuwa nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika hutazama majukumu ya kijinsia kama yanayokamilishana. Huchunguza asasi zinazomthamini na zile zinazompembeza mwanamke na kusababisha madhara kwake. Ni suala linalomfanya mwanaharakati wa mrengo wa Kiufemisti Steady (2005) kudai kuwa, bado mwanamke anapembezwa barani Afrika hata baada ya wito wa muda mrefu kutoka kwa wasomi na wanaharakati wa masuala ya jinsia kuukomesha upembezwaji wa mwanamke katika jamii. Katika kutathmini hali ya mwonoulimwengu baada ya kipindi cha miaka 30 cha kupigania ujenzi wa ujitambuzinafsia wa jinsia, Steady anasema kuwa hata katika milenia, mwanamke anazidi kupembezwa kupitia misingi inayoendana na za kirangi, kijinsia, kikabila, kitabaka pamoja kiitikadi zinazofuata mfumo wa ubabedume barani Afrika. Hii ndio maana uchunguzi huu unataka kubainisha usawiri wa suala hili katika bunilizi za Momanyi.

Kimsingi, mihimili iliyopendekezwa na Steady (1981) ni kwamba fasihi itumiwe kama jukwaa la kuielewa hali ya mwanamke kwa kuwahamasisha watunzi wa kazi za sanaa zilizo na wahusika wa kike wanaoweza kuigwa na wasiowategemea wanaume ili kujitambulisha. Kwa hivyo, ninakusudia kutumia mhimili unaosema kuwa fasihi inapaswa iwe jukwaa la kuielewa hali ya mwanamke. Hii ni kwa sababu hali ya mwanamke ni changamano sana kwa vile hutegemea mambo kama tabaka, malezi, elimu, maazimio pamoja na maingiliano.

### Utamaduni katika Upembezwaji wa Mwanamke kwenye Hadithi ya '*Ngome ya Nafsi*'

Katika hadithi fupi ya '*Ngome ya Nafsi'*, jamii anayolenga Momanyi imefungamana na kaida za kijadi kama vile tohara ya wasichana, ndoa za mapema na za kupangwa, nafasi na majukumu ya mwanamke katika jamii pamoja na taasubi za kiume. Kaida hizi humkandamiza mwanamke pindi zinapotekelezwa.

Tunamwona Naseko akishirikishwa kwenye kitendo cha tohara akiwa bado mdogo na akiwa shuleni. Naseko hafahamu athari za kukoshwa unyago katika maisha yake ya baadaye. Kama ada muhimu inayotekelezwa na wasichana wa

jamii yake, naye pia anashiriki kwayo. Moyoni mwake, anafahamu kuwa atapata nafasi ya kuendeleza masomo yake. Mwandishi anatueleza jinsi jioni moja akiwa kwenye shughuli za kuchota maji anatekwa nyara na kupelekwa kwa mume asiyemjua. Naseko anasawiriwa kwa njia ya kuonyesha jinsi wasichana wanavyoozwa mapema katika jamii ya mtunzi. Mwanamke katika jamii hii anaamuliwa mambo yanayomhusu bila yeye kutoa mchango wowote. Naseko anaangua kilio huku akidhani angepata usaidizi. Badala yake, hata wanawake wenzake wanamsimanga kwa kusema:

1. "…kilio ni cha nini sasa? Binti akisha kukoshwa unyago ya nini kumweka nyumbani? Hana budi aende kwa mumewe ati. Akikataa, hivi ndivyo afanywavyo. Au ataka mahari yarudishwe …Hebu nicheke hehe heheee!" Alisimanga… (uk. 101).

Mwanamke anaozwa kwa lazima bila kujali madhara yatakayotokana na ndoa yake. Naye anakubali na kuhatarisha maisha yake kama jinsi tunavyoona kuwa mmoja wa wake wa Mzee Sakaja alikufa akijifungua kwa sababu ya umri wake mdogo. Kuwa na mume kunachukuliwa kama jambo la hadhi kuu katika jamii na ndipo mmoja wa vijana wanaomteka Naseko nyara anambeza anapomweleza kuwa analia ilhali anapelekwa kwa mumewe. Anamkumbusha kuwa ni wasichana wengi wanaoozea majumbani wakati yeye amebahatika kupata mume na haoni hiyo ikiwa bahati. Mwanamke ni mtu wa kuolewa na kupata watoto na ndilo jambo lililomfanya Mzee Sakaja kutaka kumwoa Naseko ili amzalie watoto. Mzee Sakaja hajali umri mdogo wa Naseko ila tu anatazamia kutimiza uchu wake wa kupata watoto wengi.

### Ubabedume katika '*Ngome ya Nafsi*'

Mzee Mengo anapanga kisirisiri kumwoza bintiye Naseko kwa Mzee Sakaja ambaye ni wa umri mkubwa. Anadhihirisha ubinafsi anaotokana na itikadi ya ki-ubabedume inayotiwa nguvu na utamaduni. Mzee Mengo hataki kukiuka kanuni za jamii yake ndipo anajitahidi kutimiza ada hii. Hamhusishi mkewe katika mipango ya ndoa ya binti yao. Kama kiongozi wa familia yake, anaheshimiwa na mkewe na hivyo, kukosa upinzani kutoka kwake. Baada ya kupokea mahari, Naseko anatekwa nyara na kupelekewa mumewe. Bi. Kija, mkewe Mzee Mengo, anavunjika moyo anapopata habari za kutekwa nyara kwa Naseko. Mwandishi anasema:

2. "…Bi Kija alijipweta kitini huku machozi yakimtiririka kuwili. Akifahamu bintiye sasa ni mke wa mtu. Ijapokuwa alitaka kupinga ndoa hiyo kutokana na tabia za Mzee Sakaja, mumewe alikwisha kuamua hatima ya Naseko…" (uk. 103).

Badala ya kujadili masuala kuhusu familia yao kwa pamoja kama mume na mke, Mzee Mengo amejukumishwa na utamaduni wake kuwa mwamuzi wa masuala ya familia yake bila kumhusisha mkewe. Tunaweza kusema kuwa,

alikuwa ameikamilisha mipango yote ya kumwoza bintiye yeye binafsi pasi na mchango wa mtu mwingine katika familia hiyo. Jukumu la kumchagulia Naseko mchumba linatimia. Anahitaji mahari kutokana na mabinti zake na alikuwa amekwisha ipokea. Mbali na hayo, Mzee Sakaja anamletea mifugo wengi na linalobaki ni kutekwa nyara kwa Naseko na kupokezwa kwa mumewe. Mzee Mengo anajua hakuna anayeweza kumuuliza kwa uamuzi wa kumwoza Naseko. Hata chifu, kama mwakilishi wa serikali, anaungana na wanaume wa jamii husika kutekeleza mila potovu zinazompembeza mwanamke zikiwemo ndoa za mapema tena za kupangwa na wazazi. Badala ya chifu kuwa mstari wa mbele kupinga desturi hizi kandamizi, zinaendelezwa bila yeye kuwachukulia wazazi husika hatua za kisheria.

Mzee Sakaja anathamini idadi kubwa ya watoto na ndio sababu anaamua kuoa wake wengine wa kumzalia watoto na hasa baada ya mke wake wa kwanza kushindwa kupata watoto. Baada ya kumwoa Bi Ngunga, anawaoa wengine wanne. Ni baba wa mtoto mmoja Idi, aliyemzaa na Bi Ngunga. Ni mzee aliyebobea ubinafsi na ukatili. Anataka kudumisha sifa yake kijijini kwa kuwa na idadi kubwa ya watoto. Shauku ya kupata watoto inamfanya kumtishia mke wa pili talaka kwa utasa. Mzee Sakaja ni kiwakilishi cha wanaume katika jamii wanaomwonea na kumdunisha mwanamke tasa. Anampembeza mke wake na kumdunisha kwa kukosa mtoto. Anaonyesha mtazamo wa jamii kuhusu mwanamke tasa; kuwa anastahili kutalakiwa na kumwooa mwingine. Mwanamke anajengewa ujitambuzinafsia hasi unaompembeza kwa kukosa uwezo wa kupata mtoto.

Mwandishi anatumia Mzee Sakaja kudhihirisha jinsi mfumo wa ki-ubabedume unavyotekeleza maovu dhidi ya mwanamke. Mfumo wa ki-ubabedume hautambui madhara yanayosababishiwa mwanamke kupitia ndoa za mapema. Kifo cha msichana wa shule anayefia kwa Mzee Sakaja kinawakilisha uangamizi wa kizazi cha kike. Hawapewi nafasi kunawiri kimaisha. Nguvu na uwezo anaopewa mwanamume na utamaduni unamfanya Mzee Sakaja awe na azma ya kumwoa Naseko baada ya kifo cha msichana mwenzake. Tabia ya Mzee Sakaja ni kiwakilishi cha udumishwaji kupitia utamaduni hasi unaowasababishia wake zake mateso ya kisaikolojia. Ni mfano wa wanaume wanaowapembeza wanawake na kuwajengea ujitambuzi hasi kwa kuwa utamaduni jadi na mfumo wa ki-ubabedume, unaiona jinsia ya kike kuwa ‘wengine’ katika jamii.

### Kujikandamiza kwa Mwanamke katika Hadithi ya ‘*Ngome ya Nafsi*’

Mwandishi anatumia Bi. Kija kuonyesha vile mwanamke anajikandamiza mwenyewe. Bi. Kija anakubaliana na kauli za mumewe hata kama zina madhara kwa watoto wao. Kwa mfano, mifugo wanaletwa nyumbani kwake na Mzee Sakaja kama mahari ya Naseko na hapingi. Ingawa anafahamu jinsi Mzee Sakaja anavyowadhulumu wake zake, hamkanyi mumewe dhidi ya mipango yoyote ya ndoa ya mwana wao. Naseko anapomuuliza sababu ya kuletwa kwa mifugo,

anamdanganya kwa kumwambia kuwa waliletwa hapo kwa muda tu ili mwenyewe apate nafasi ya kujenga zizi kubwa zaidi la kuwasitiri (uk. 106).

Fauka ya hayo, tunamwona Bi. Kija akiwa amepofushwa na mila na desturi kiasi cha kumfanya kukosa kumweleza kinagaubaga kuwa, yeye Naseko, ndiye sababu ya mifugo wale kuletwa. Hamwelezi kuwa ndiye anayeozwa kwa Mzee Sakaja. Hamtayarishi kisaikolojia kuwa angefanywa mke wa mtu kwa lazima. Iwapo angemweleza, huenda Naseko angejinusuru mapema. Kama mwanamke, ingefaa zaidi ikiwa angemtayarisha bintiye kwa majukumu yaliyokuwa mbele yake. Badala yake, anajifunga kwenye ngome ya nafsi yake mwenyewe na kujipembeza binafsi huku mumewe akimpembeza zaidi. Anakubali mila na desturi kandamizi kumtawala na kuwaingiza wasichana wake katika wavu huo wa utamaduni uliopitwa na wakati.

Isitoshe, Bi. Kija anafahamu fika tabia ya Mzee Sakaja za kuwatandika wake zake kutikana na hamaki kwa makosa madogomadogo. Mbali na kufahamu tabia za mzee huyu, bado anamruhusu bintiye kaolewe na mzee huyo ili aendeleze utawala wa ki-ubabedume katika ndoa yake. Bi. Kija ametiwa ububu na mumewe na kukosa kuiona nafsi yake. Anapopokea habari za kutekwa nyara kwa Naseko kutoka kwa ndugu zake, hachukui hatua yoyote ya kumnasua. Anasema;

3. “Naelewa kilichotokea, nitawaeleza baadaye…Alijitoma chumbani na kuufunga mlango, huku akiwaacha wanawe wakitazamana kwa mshangao. Bi. Kija alijipweteka kitini huku machozi yakimtirika kuwili. Alifahamu bintiye sasa ni mke wa mtu. Ijapokuwa alitaka kupinga ndoa hiyo kutokana na tabia za Mzee Sakaja, mumewe alikwisha kuamua hatima ya Naseko. Alichofanya yeye ni kukubali matakwa ya mumewe ambaye hakutaka ushauri wowote kutoka kwake.” (uk. 103).

Mbali na hayo, Bi. Kija ametiwa kimya cha lazima na kujengewa ujitambuzi hasi anaojengewa na jamii yake. Badala ya kujitahidi kumkomboa binti yake, anaingia chumbani na kulia. Anafahamu bayana hali ya maisha wanayopitia wake za Mzee Sakaja. Anajua fika kuwa bintiye wa umri mdogo anaenda kuwa mke wa tano wa Mzee Sakaja. Inasikitisha kuona kuwa, mbali na ukweli huu, Bi. Kija hachukui hatua yoyote ya kumnasua binti yake kutoka katika mtego huo. Kama wanawake wengine kijijini, anakubaliana na maamuzi ya wanaume hata kama yanaathiri maisha yao kama kundi linalonyanyaswa. Wanawake hawa wanaridhishwa na hali ya kupembezwa kwa kutengewa nafasi ya kuzaa na kulea watoto huku wanaume wakiachiwa kufanya maamuzi ya watoto hao na ya wake zao kama viongozi wa familia. Ukubalifu huu unaonyesha kuwa mwanamke anajikandamiza yeye mwenyewe kwa kukosa kupigania haki zake kadri ya uwezo wake. Bi. Kija hataki kugombana na mumewe kwani ugomvi kama huo ungemsababishia talaka. Hivyo, anawaachilia wasichana wake wateseke chini ya mila potovu. Tunamwona Naseko akiwaza juu ya wasichana ambao wanakosa uwezo wa kutoroka kama yeye. Anasema kuwa wanaishi kama wafungwa

wanaojikandamiza kwa kukosa kutetea haki zao za kibinafsi. Kinyume na mamake, Naseko anapinga upembezwaji dhidi ya mwanamke kwa kujijengea ujitambuzinafsia chanya na wa jinsia ya kike.

**Ubabedume katika riwaya ya *Tumaini***

Katika sehemu hii, nitaangazia athari za utamaduni na ubabedume katika upembezwaji wa jinsia katika jamii. Utamaduni ni jumla mila na desturi zilizotengewa kila mwanajamii. Kila jamii huwa na kanuni zinazoiongoza ili kukuza utangamano na umoja kwa ajili ya kuendeleza maendeleo na wiano miongoni mwa wanajamii. Vipengele vya utamaduni na ubabedume huthihirika na kuathiri wanajamii katika asasi za jami kama ndoa, dini na taasisi za elimu miongoni mwa nyingine. Asasi hizi huchangia ubabedume kwani ndizo nguzo muhimu za familia. Millet (1977) anasema kuwa ndoa ndiyo asasi kuu inayoendeleza ubabedume. Kutokana na ndoa, tunapata familia. Familia huimarisha ubabedume kwa kuwa huongozwa na wanaume. Hivyo nitaangazia jinsi kaida za jamii na mfumo wake zinavyotumika kudumisha upembezwaji wa mwanamke hasa kupitia asasi za ndoa.

Mzee Masumbuko ni mumewe Bi. Amina na babake Tumaini, Rehema, Mashaka na Idi. Ni mtu anayetumika kama mwakilishi wa utamaduni na ubabedume katika riwaya ya *Tumaini*. Anashikilia desturi kandamizi hivi kwamba, habadilishwi na mpito wa wakati au mtu yeyote yule. Ni mhafidhina wa kiwango cha juu ambaye amening'inia na kufuata mila zilizopitwa na wakati kama vile tohara za wasichana na ndoa za mapema tena za kupangiwa. Utamaduni wa jamii yake umempa uwezo ambao unamfanya kuiongoza familia yake kwa ubaguzi wa kijinsia. Anaidhalilisha jinsia ya kike huku akiitwaza ya kiume kiasi cha kuwachapa mabinti zake kwenye gunia la jani la upupu kwa makosa madogomadogo. Tumaini anahofia kurudi nyumbani baaada ya kutoroka kwa kukumbushwa na Idi jinsi babake alivyokasirika. Tunasoma; *"Baba amekasirikaTuma! Alimwambia Mashaka amtayarashie gunia tupu kisha akachukua panga na kuelekea shambani," Idi alisema. "Jani la upupu!"Alitamka Tumaini*. (uk. 28).

Mzee Masumbuko anathamini mtoto mvulana; Idi kwa kuwa ataendeleza kizazi cha ukoo wake. Anamdekeza na kumfanya ahisi kuwa yeye Idi, ni tofauti na nduguze wa kike. Malezi anayompa Idi yanamfanya yeye Idi awadhalilishe dada zake na kumkosea heshima Tumaini ambaye ni dada yake mkubwa. Tunasoma;

4. '…Kauli za Idi zilimkera Tumaini kwa muda mrefu. Kila mara alimkabili na kumkumbusha babake kuwa lugha aliyoitumia dhidi yao ilikuwa inamwathiri vibaya kakake mdogo. Babake alimkera na kumkanya kutoingilia malezi ya Idi kwani yeye ni mtoto wa kiume si wa kike. Aidha, alihitaji moyo mgumu kama yeye ili kuyakabili maisha'… (uk. 14).

Ninaweza kuhoji kuwa Mzee Masumbuko anamtarajia mwanamume kuwa na moyo mgumu usio na huruma kwa mwanamke. Moyo unaoweza kumchukulia

mwanamke kama kiumbe duni bila kuheshimu haki zake za msingi. Mzee Masumbuko hajali kuhusu machungu anayowasababishia wanawake. Anaishi katika ulimwengu wa jadi mbali na mabadiliko yanayomzingira. Msimamo wake unakinzana na wa Tumaini pamoja na Bi Halima kwa kusema kuwa Tumaini hangekuwa msungo na tohara kwake ni lazima. Lau angekosa kufanya hivyo, basi hangeruhusiwa kuishi nyumbani kwake. (uk. 39).

Mzee Masumbuko anashikilia uhafidhina kiasi cha kumtelekeza bintiye kwa kukaidi amri yake ya kupashwa tohara. Isitoshe, uhafidhina unamfanya kutotishika hata baada ya tishio la kuchukuliwa hatua za kisheria na Bi Halima pamoja na mzee Yusufu. Anapanga kisirisiri kumwoza Tumaini akiwa bado mwanafunzi wa darasa la saba na anayetia fora masomoni. Anaenda kumtafutia mchumba kutoka mbali Maunguja kwani anahofia watu wa karibu wangesusia kumwoa kwa ajili ya usungo wake. Anamwendea mwandani wake wa kibiashara, Selemani Bin Mabruk ili kumposea binti yake aliyeghairi mipango ya kupashwa tohara. Mzee Masumbuko ni mhusika anayejawa na hamaki na usumbufu mwingi kwani anaamini kauli yake kama mwanamume, ndiyo ya mwisho kulingana na mila na desturi za jamii yake.

Uamuzi wa Tumaini wa kukaidi mipango ya babake, Mzee Masumbuko, ya kumpasha tohara ni pigo kuu kwa babake,utamaduni na mfumo wa ki-ubabedume. Kama mila na desturi za jamii yake, tamaduni, anahisi kuwa nafasi yake kama kiongozi wa familia inadunishwa. Anaona kuwa anashushiwa hadhi katika ukoo wake kwa kuwa, hakuna hata mzee mmoja asiyewatahirisha mabinti zake. Hivyo, anataka kuficha aibu ya kuwa wa kwanza kwenye ukoo wake kuwa na msungo (uk. 52). Anaposhindwa kumwoza bintiye, hakati tamaa ila anazidi kumkandamiza na kumjengea ujitambuzinafsia hasi. Anamwendea Chifu Andrea na kumzawadi ili amnyime Tumaini ufadhili wa serikali wa kuendelea na masomo yake. Hataki bintiye aendelee na masomo. Anataka kumwoza ili afaidi mahari.

Mipango ya Mzee Masumbuko kumhusu Tumaini inapoambulia patupu, anamwoza bintiye Mashaka kwa lazima kwa Mzee Lusimbo kama mke wa tatu. Anamsababishia huzuni. *'...kwa sababu ya madhila hayo, ufyefye ulimvaa Mashaka, vibega vikainuka juu kama vya ndege…* '(uk. 123).Tamaa ya Mzee Masumbuko inamfanya kukosa kuona umuhimu wowote wa mtoto wa kike ila kuwa chanzo cha kupata mahari. Anamtelekeza Tumaini na kusema kuwa, ingawa ni mwerevu, hilo halimfaidi. Fahari kwake ni kumwoza na kupata mahari. Elimu haingemsaidia chochote. Hisia zake hasi kuhusu msichana ndizo anamridhisha Idi na kumfanya amdharau Tumaini kwa kumwambia, " *Naam. Ala! Mbona hivyo. Si umemaliza shule. Ni lipi linabaki kama si ndoa*?"(uk. 128) Anamtayarisha Idi kuwa mgumu kama yeye na kufuata mila na desturi za jamii yake bila kubanduka.

Madharau ya Idi kwa dada zake yanasababishwa na mfano anaouiga kutoka kwa babake Mzee Masumbuko ambaye ni mwakilishi wa utamaduni jadi na ubabedume. Anawakatizia binti zake masomo na hivyo, kuashiria upembezwaji wa

mwanamke. Kupitia kwake, jinsia ya kike inaangamizwa. Iwapo kizazi cha kike kitapata nafuu, lazima pawe na watetezi na wakombozi kama Tumaini, Mwalimu Mwandime na Bi Halima wanaopigana na mila zinazompembeza mwanamke. Mzee Masumbuko anatiwa nguvu na mazingira ya kijijini ambako tohara kwa wasichana na ndoa za kupangwa na za lazima zimekita mizizi.

**Utamaduni wa Jamii katika Riwaya ya *Tumaini***

Jamii ya Tumaini inazingatia mila na itikadi zilizopitwa na wakati. Miongoni mwa itikadi hizi ni tohara kwa wasichana. Utamaduni huu unapitishwa kwa kila mwanajamii kupitia malezi na utekelezwaji wa utamaduni husika. Watoto wanapokezwa utamaduni hasa na wakubwa wao. Kila mwanajamii anapaswa kutimiza ada husika. Mbali na hali ya nyumbani kwa kina Tumaini, mazingira ya shuleni pia yanakuwa magumu kwake kwa kukosa kutimiza ada ya kupashwa tohara. Kutoroka kwake nyumbani kunachukuliwa kama hali ya kukosa ujasiri wa kutimiza ada za jamii. Ukaidi wa Tumaini wa kupinga tohara na ndoa ya mapema unamfanya kudunishwa na marikaze wanaozingatia ada hizi potovu. Wanamwona kama mwoga. Wanafunzi hawa wanamkejeli na kumsimanga kama inavyojitokeza kupitia kwa mmoja wao kwa jina Kijungwe. Anamwambia;

5. “Tuma, hivi ulikimbia tohara kwa sababu ya woga au mchumba uliyechaguliwa hukumpenda? Nasikia ulichana mbuga hadi kwa mamako mdogo. Nilidhani wewe ni msichana jasiri sana wala hungeogopa kisu. Au ni wembe?” (uk.72).

Kauli ya Kijungwe ni dhirisho la upembezwaji dhidi ya mwanamke katika jitihada za kujijengea ujitambuzinafsia katika jamii. Kijungwe ni kielelezo cha wavulana wanaowavunja wasichana moyo na kuwavunjia heshima yao hasa wanapodhihirisha misimamo chanya kuhusu maisha. Masimango haya yanaonyesha jinsi jamii inavyomtenga na kumvunja moyo yeyote anayakwenda kinyume na ada zake. Anadharauliwa na kupembezwa kwa kwenda kinyume na ada na matarajio yake. Tumaini anaonyesha msimamo usiotetereka unaopingwa hata na wanafunzi wenzake wanaozingatia mtazamo jadi kuhusu mwanamke. Mbali na masimango, Tumaini anatia masikio komango ili maneno ya wanafunzi wenzake yasiathiri bidii yake masomoni.

Isitoshe, Sifa, mwanafunzi mwenzake, anaimjia kwa njia tofauti na Kijungwe. Sifa hamkejeli ila anampembeza kwa kumtazama kama chombo cha kutimiza uchu wa mapenzi katika umri wao huo mdogo. Anamjengea Tumaini ujitambuzinafsia hasi kwa kumwandikia barua. Tumaini haruhusu uhusiano wa kimapenzi na wavulana. Anaipeleka barua hiyo kwa Mwalimu Mwadime. Tumaini hapendezwi na jinsi Sifa anavyomfananisha na twiga na kitumbua. Sifa anamdunisha kwa kumchukulia kama mpenzi wa kuchezea atakavyo. Mwandishi anamsawiri Sifa kama kielelezo wavulana wanaofuata utamaduni wa kuwachukulia wasichana kama vyombo vya starehe. Ujasiri wa Tumaini unamfanya Sifa kuadhibiwa ili

kukomesha tabia ya uhusiano wa kimapenzi miongoni mwa wanafunzi kwa kuwa huathiri masomo yao.

Fauka ya mazingira ya shuleni, Tumaini anatafuta kazi kwa Bi. Selina mkewe Chifu Andrea. Nyumbani kwa chifu huyu, Tumaini anakabiliana na Chifu mwenyewe pamoja na mwanawe Majuto katika jarabio la kumbaka. Anapigana nao ili kudumisha heshima ya kibinadamu. Chifu Andrea na Majuto ni wawakilishi wa ubabedume unatiwa nguvu na utamaduni katika jamii. Wanaume wenye mwelekeo huu hutumia tofauti za kimaumbile kumkandamiza mwanamke. Chini ya mtazamo huu, mwanamume anajichukulia kuwa na uwezo zaidi ya mwanamke. Tumaini hayuko tayari kuchukuliwa kama wajakazi wengine waliotumiwa vibaya na Chifu Andrea. Bi. Halima anamfokea Bi. Selina anapomwambia;

6. “Ni wasichana wangapi mumeo amewaharibu mitaani, wengine hata akiwasaidia kuavya?...Vigoli wangapi wameajiriwa kazi hapa kisha wakatoka na mayowe, mikono vichwani?” (uk. 95).

Kauli ya Bi. Halima inadhihirisha jinsi ubabadume unavyomfanya Chifu Andrea kuwadhulumu wasichana kingono. Tumaini anakataa katakata kunaswa na mtego wa Chifu huyu dhalimu. Anajinasua na kurudi kwa mamake mdogo. Kukosa kumtimizia Chifu Andrea uchu wa kimapenzi kunazua uhasama dhidi yake. Chifu Andrea analipiza kisasi kwa kushirikiana na Mzee Masumbuko, mhafidhina mwenzake kumnyima ufadhili wa masomo. Mzee Masumbuko anajaribu juu chini kuhakikisha kuwa Tumaini hafadhiliwi ili kuyatamatisha masomo yake. Hataki Tumaini afaulu hasa baada ya kukaidi amri zake. Anampiga vita na kuhakikisha hapati haki anayostahili.

Anapojiunga na shule ya upili, anajibiidisha katika masomo asije akawaaibisha wafadhili wake. Anafanya vyema zaidi katika masomo ya sayansi. Mbali na kuzawadiwa *Junior Science Cup*, *Senior Science Cup* na *Languages Cup*, mwalimu Majaaliwa hakuamini kuwa angefaulu katika masomo ya sayansi. Mwalimu Majaaliwa, kama mwanamume yeyote aliyeathiriwa na utamaduni kuhusu ujitambuzinafsia wa jinsia, haamini jinsi msichana anavyoweza kufaulu katika masomo haya. Anampembeza Tumaini kijinsia na kumwambia asije akachagua kozi za sayansi kwenye chuo kikuu. Anamwambia Tumaini; *“Nimesema masomo ya sayansi yasijazwe. Nyie wasichana ni vigumu sana kufuzu katika masomo haya.Kwanza, ni wasichana wanagapi umeskia hufuzu udaktari chuo kikuu, eeh?”* (uk. 115).

Mwandishi anamtumia mwalimu Majaaliwa kuonyesha jinsi jamii inavyomdunisha mwanamke na kumpembeza kikazi. Wanaume hutengewa kozi zenye hadhi. Isitoshe, jamii imekuwa mstari wa mbele kumwamulia mwanamke mambo ya kufanya. Mwanamke ananyimwa nafasi ya kufanya uamuzi kuhusu mambo anayotaka kufanya yakiwemo kazi katika vyuo vikuu. Tumaini anakataa kuamuliwa maisha yake na kuirudisha fomu ikiwa haijajazwa. Anamkabili mwalimu Majaaliwa na kumwambia kuwa anajiamini na hivyo angechagua

masomo ya sayansi. Hatua ya Tumaini ya kumkabili mwalimu wake inaonyesha ukakamavu na ukomavu wa kimawazo wa mwanamke. Mwanamke ana shauku ya kupigania anachotaka maishani na ana uwezo sawa na wa mwanamume wa kutekeleza majukumu katika jamii. Katika nyanja zote za maisha ya binadamu, kila mja ana uwezo sawa wa kushiriki kwenye maendeleo ya jamii mbali na tofauti za kimaumbile ingawa atapewa nafasi hiyo.

Bi Halima anafahamu juhudi zinazofanywa na jamii katika vita dhidi ya utamaduni kandamizi. Ni jambo linalomtia nguvu anapopambana na kusudio la Mzee Masumbuko la kumpasha tohara Tumaini. Anaelewa kuwa, jamii imehamasishwa kuasi mila kandamizi na kumpa mwanamke nafasi yenye staha katika jamii. Anaamini kuwa wanaume wanaofuata mambo ya kale wanapigana na upepo wa mabadiliko. Hatimaye, wataambulia patupu kwa kuwa kupigana na mabadiliko ni sawa na kupiga ngumi ukuta (uk. 24). Wahafidhina kama Mzee Masumbuko hawafiki mbali katika jamii inayopigania ujitambuzinafsia chanya wa mwanamke. Ni bayana kuwa hawakuweza kumtahiri Tumaini wala kukatiza masomo yake. Ni ushindi kwa watetezi wa haki za watoto wa kike wakiwemo Bi. Halima kwa kufaulu kumnasua Tumaini. Ikiwa msichana ana ari ya kusoma, inamaasha kuwa angesaidiwa na jamii ya kisasa kutimiza ndoto yake.

Zaidi ya hayo, Bi. Halima anashirikiana na familia yake kukatiza mipango ya kumwoza Tumaini akiwa bado shuleni. Wanavamia Mzee Masumbuko na kuvuruga kikao kilichofanywa kujadili posa ya Tumaini. Tunaweza kusema kuwa, hi ni ishara ya muungano wa jamii katika muungno wa nguvu na ufanisi dhidi ya vita vya ukomboziwa mwanamke. Mipango ya Mzee Masumbuko inasambaratika na Tumaini anapata afueni. Anaendelea na masomo kuwa utulivu na kutimiza ndoto yake.Mbali na vita dhidi ya utamaduni kandamizi, Bi Halima anapigana na udhalimu kwa mtoto wa kike na hasa ubakaji. Anamwendea Bi. Selina kwa ukali na kukashifu kitendo cha Chifu Andrea cha kujaribu kumbaka Tumaini. Yuko tayari kupambana na Chifu mwenyewe. Anamwambia kwa ukali, "*Basi mwambie, akazidi kumchezea mwanangu Tuma, nitamvua huo uchifu akajikuta taabani*." (uk. 96).

**Ubabedume katika Riwaya ya *Tumaini***

Mzee Masumbuko anakula njama na Chifu Andrea kuliondoa jina la Tumaini kwenye orodha ya wanafunzi wanaohitaji kufadhiliwa kimasomo. Tumaini anapigania haki yake anapovamia ofisi ya D.O. na kufuatiliza ufadhili huo. D.O. anamtegea sikio na kukasirishwa na ubaguzi dhidi yake. Haelewi kwa nini Chifu Andrea analiondoa jina la Tumaini kwenye orodha. Anasema;

> 7. "*This is bad,really bad*…Bwana chifu, ningependa utwambie kwa nini umeleta majina ya mwanafunzi wanne badala ya watano na useme ukweli chifu maana hakuna mzaha hapa."(uk. 102).

Kauli ya D.O. inaashiria umuhimu ambao serikali imetia katika kupiga vita ubabedume ili kupata ufanisi wa jinsia ya kike. Vilevile, ni hatia kumbagua na

kumnyima haki mtoto kwa msingi wa jinsia yake. Ikiwa Tumaini hakujipeleka mwenyewe kwenye kikao, ufadhili wake ungepotea. Anayejukumishwa na serikali kuwatendea wananchi haki ndiye anaikanyagia chini. Ni wanafunzi wengi wanaodhulumiwa jinsi hii na kukatiziwa ndoto zao za masomo, kufuatia udhalimu wa viongozi wa mashinani. Waliopewa wajibu na serikali wa kuhakikisha mtoto amepata masomo wanatumia nyadhifa zao kumkandamiza.

D.O. anajukumika kumlinda mtoto wa kike dhidi ya dhuluma zinazompembeza na kumjengea ujitambuzinafsia hasi. Kama kiongozi wa serikali, anaunga sera za serikali mkono kwa kuihamasisha jamii kuhusu madhara ya ubabedume pamoja na uzingativu wa mila kandamizi. Ndio maana anamwita Mzee Masumbuko ofisini mwake na kumwonya kutoingilia elimu ya mwanawe Tumaini. Anamhakikishia kumchukulia hatua za kisheria endapo angeenda kinyume na masharti yake. Isitoshe, anamtishia Chifu Andrea kupoteza wadhifa wake iwapo angezidi kushirikiana na wahafidhina kama Mzee Masumbukokatika kuhujumu ujenzi wa ujitambuji chanya wa mwanamke. Msimamo wa D.O. unaleta mwanga katika jamii kwa kukomesha upembezwaji wa mwanamke na kumpa nafasi ya kujiendeleza.

Mbali na kuwa ni jukumu la vyombo vya utawala kulinda mwanamke dhidi ya ubabedume, walimu nao wanatambua vipawa vya wanafunzi wao na kuvipalilia ili kuwafaidi siku za usoni. Isitoshe, ni jukumu la walimu kuhakikisha kuwa mazingira ya shuleni yanafaa kwa shughuli za masomo kuendelea. Mwalimu Mwadime anadumisha nidhamu shuleni mwake na kuhakikishia kuwa, kila mwanafunzi anapata fursa nzuri ya kusoma. Ndiyo sababu anamwadhibu Sifa anapomwandikia Tumaini barua ya mapenzi. Anajua ikiwa tabia hio ingeruhusiwa shuleni, ubora wa masomo ungeshuka. Anashika hatamu ya kuwaunda wanafunzi wanapokua ili kuwa na uhusiano wa kutagusana kimwanafunzi wala sio kimapenzi. Inamfahamikia kuwa uhusiano wa kimapenzi kati ya wanafunzi wa umri huu ungewapotosha kimaadili na kuathiri vibaya masomo yao. Isitoshe, anamsaidia Tumaini kupata ufadhili ili aweze kusoma sawia na wenzake wavulana. Anatambua uwezo na bidii ya Tumaini na hivyo, kumtakia mema siku za usoni. Analiorodhesha jina lake kati ya majina ya wanafunzi wanaohitaji ufadhili. Mbali na hayo, anamfafanulia D.O. kuwa orodha aliyompa chifu ilikuwa na wanafunzi watano. Anaingilia kati kuhakikisha kuwa Tumaini anaendeleza masomo na habaguliwi kwa msingi wa jinsia yake.

## Hitimisho

Makala haya yamebainisha kuwa mwanamke amezingirwa na vizingiti vingi mambo yaliyo nje ya uwezo wake, na ambayo mambo hayo ndiyo huelekeza maisha yake. Haya ni pamoja na mfumo wa kijamii ambao unadhibitiwa na mwanamme. Mwanamume ndiye huendesha kila kipengele cha maisha ya jamii, mwanamke akiwapo. Aidha, mwanamume ndiye anauunda utamaduni kwa namna ambavyo utamfaa yeye. Kwa kufanya hivyo, anamuumiza mwanamke. Huku ni

kusema kuwa, utamaduni kama kizingiti cha mwanamke ni zao la mwanamme. Utamaduni huu ndio umemfunza mwanamke kuwa mnyonge, kwa jinsi hiyo yeye kuchukua nafasi ya pili kila mara.

**Marejeleo**

Bank, O. (1990). *Faces of Feminism. A study of Feminism as a Social Movement.* USA: Basil Blackwell

De Beauvoir, S. (1949). *The Second Sex*. London: Pan Books Publishers.

Eagleton, M. (1991). *Feminist Literary Criticism - Woman in Literature.* London: Longhorn Publisher.

Lugano, R. S. (1989). *Mwanamke katika Riwaya za Kezilahabi.* Gainesville: Florida University Press.

Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi na Nadharia.* Nairobi: Standard Text Books Graphics and Publishing.

Millet, K. (1997). S*exual Politics.* London: Virago Press.

Momanyi, C. (2006). *Tumaini.* Nairobi: Vide – Muwa publishers.

Muindi, A. (1990). "Usawiri wa Wahusika Makahaba Katika Riwaya za S.A Mohamed". Tasnifu ya Uzamifu Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Musyoka F. M. (2011). 'An Analysis of the Woman in Gender Role - Play Dynamics in Kenyan Kiswahili Drama.' Tasnifu ya Uzamifu Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa.)

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji Wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Steady, F. C. (1981). *Reflecting on the Politics of Sisterhood.* New York: African Wordpress.

Steady, F. C. (2005). An Investigative Framework For Gender Research In Africa In The New Millennium. *In African Gender Studies* A Reader (pp. 313-331). Palgrave Macmillan, New York.

Swaleh, A. (2011). "A Critique of the Mapping and Construction of Gender Identity and Authority in the Selected Kiswahili Novels". Tasnifu ya PhD Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa.)

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: Phoenix Publisher.

Wamitila, K. W. (2004). Mayai waziri wa Maradhi ma Hadithi Nyingine. Nairobi: Phoenix Publisher.

Wollstonecraft, M. (1792). *A Vindication of the Rights of Woman.* London: Blackwell Publishers.